# MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA (THRDC)

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUVAMIWA NA KUPIGWA KWA WAANGALIZI WA UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA KWA NJIA YA MFUMO MPYA WA TEKNOLOGIA YA ALAMA (BVR) – MJINI MAKAMBAKO

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unapenda kuwatahadharisha watetezi wote wa haki za binadamu pamoja na mashirika yanayo au yatakayojihusisha na uangalizi wa uchaguzi mwaka huu kuzingatia sana suala la usalama. Angalizi hili kwa watetezi linakuja wiki kadhaa baada ya waangalizi wa uandikishaji upya wa daftari la wapiga kura Mkoani Njombe kuvamiwa hotelini na kupigwa na watu waliojulikana baadaye kuwa ni askari wa Jeshi la Polisi.

Hata hivyo THRDC pamoja na Mtandao wa Mashirika ya Uangalizi wa Chaguzi -TACCEO tunashukuru Jeshi la Polisi Makao Makuu kwa kutoa ushirikiano wa kutosha katika suala hili hadi kuunda Tume ndogo ya uchunguzi wa tukio la kuvamiwa na kudhalilishwa na polisi waangalizi wa uandikishaji wa wapiga kura kwa njia ya BVR waliokuwa wakifanya kazi chini ya TACCEO Mjini Makambako, Mkoani Njombe.

Mtandao wa watetezi wa haki za binadamu ni Mtandao wenye wanachama zaidi ya 100 na kazi yake ni kutetea watetezi wa haki za binadamu nchini kote kwa kufanya watambulike kisheria, kuwajengea uwezo na kuwalinda kwa namna mbali mbali pale haki zao zinapovunjwa sababu ya kazi zao za utetezi.

TACCEO ni MTANDAO wa Asasi za Kiraia wa Kuangalia Chaguzi Tanzania, Mtandao huu umetuma waangalizi katika wilaya zote nchini ili kuangalia uandikishaji wa wapiga kura kwa kutumia Mfumo mpya wa Teknolojia ya Alama (BVR). TACCEO chini ya Uongozi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) imepewa mamlaka na Tume ya Uchaguzi (NEC) kuwa mwangalizi wa ndani wa Undikishaji wa wapiga kura kwa njia ya BVR. TACCEO ilituma waangalizi sita (6) kwa majina Grace Mwangamila, Amina Uddi, Jackline Simkanga, Humphrey Josiah, Wilson Raphael, na Samuel Stanley mnamo tarehe 21 February, 2015 kwenda Makambako ambapo uandikishaji wa wapiga kura unatarajiwa kufanyika kwa siku takriban 28 kuanzia Februari February 23mpaka March 25, 2015 katika vituo 87 ndani ya kata 12.

## KUVAMIWA NA KUPIGWA KWA WAANGALIZI WA BVR

Waangalizi wa TACCEO Makambako Bw. Humphrey Josia na Wilson Raphael siku ya tarehe 7 mwezi Machi 2015 mnamo saa Nne na dakika arobaini na tano usiku wakiwa katika chumba namba 5 cha Netho Guest House wakiandika repoti ya kazi za siku walivamiwa na

polisi sita walio kuwa na silaha. Walipigwa bila huruma huku wakituhumiwa kuwa ni majambazi. Waangalizi hawa walidaiwa kuiba laptop sita (6) mjini Mafinga Mkoani Iringa na hivyo kupigwa bila huruma hadi kuumizwa.

Waangalizi hawa ambao waliingia Mkoani hapo mnamo tarehe 22 mwezi wa pili mwaka 2015 na kufuatilia taratibu zote za kureport police, hawakusita kutoa taarifa za kuvamiwa na kupigwa katika kituo hicho cha Makambako , Ingawa watuhumiwa walikiri kosa na kuomba radhi kituo husika pamoja na uongozi wake wa juu hawakutoa ushirikiano kuhakikisha polisi hao wahalifu wanawajibika kwa makosa yao. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilijitahidi kuwasliliana na Mkuu wa Kituo cha Polisi Makambako lakini hakukuwa na ushirikino wenye kuzingatia vitendo vilivyofanywa na askari hao.

Hadi sasa hali za wahanga wa tukio hili inaendelea vizuri, ila shughuli zote za uangalizi wa zoezi la uandikishaji wa wapinga kura limesimamihshwa chini ya Uongozi wa TACCEO kutoa muda wa tathmini wa masuala ya usalama. Hivi wahanga wa vipigo vya polisi wameshafungua malalamiko yaliyosajiliwa Mjini Makambako kwa kumbumbuku namba *Makambako (MKB/IR/384/2015)* dhidi ya polisi wanaotuhumiwa kuwavamia, kuwapiga na kuwadhalilisha waangalizi wa BVR.

**USHIRIKIANO WA JESHI LA POLISI MAKAO MAKUU**

Kutokana na kukosa ushirikiano wa awali kutoka kwa ngazi za kituo cha polisi husika, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu baada ya kuwa na kikao cha dharura tarehe 10/3/2015 uliwasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa lengo la kuwapa taarifa kamili na kuwasihi wawachukulie hatua wahusika.

Tunamshukuru sana Makamu wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Abdulrahman Kaniki kwa kuonyesha ushirikiano wa dhati katika suala hili. Jeshi la Polisi Makao makuu limezingatia jitahada za kuboresha mahusiano kati ya makundi ya haki za binadamu na Jeshi la Polisi unaofanywa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu kwa kuamua kuunda Tume ndogo ya kulifuatilia suala hili kwa undani kabla ya kulitolea maamuzi.

Mtandao unalipongeza Jeshi la Polisi kwa ushirikiano huu, ila tunaomba hatua zitakazochukuliwa dhidi ya askari hao zifahamike kwa umma ili kuzuia vitendo kama hivi kujirudia katika maeneo mengine na katika shughuli zingine za uchaguzi zinazotegemewa kufanyika mwaka huu.

**WITO WETU:**

a) **Kwa polisi**
    i. Viongozi wa ngazi za juu katika vituo cha polisi nchini waache kutetea uovu wa askari wasiozingatia maadili ya kazi zao,
    ii. Tunaisihi timu ya uchunguzi Makao Makuu ya Polisi Ifuatilie suala hili kwa huaraka na kuarifu umma hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari hao,
    iii. Tunawakumbusha askari polisi hasa mwaka huu tunapoelekea kwenye uchaguzi kutambua kuwa wao pia wanatakiwa kuwa watetezi wa haki za binadamu na hivyo wanajukumu la kuzilinda haki kwa kufanya kazi yao kwa mujibu wa sheria.

iv. Kuhakikisha ulinzi kwa waangalizi wa ndani na wa nje wakati wa uandikishwaji wa majina kwenye kitabu cha kudumu , kura za maoni na uchaguzi mkuu.

**b) Kwa Watetezi wa Haki za Binadamu**

i. Tunaendelea kusisitiza kuwa wale watakaoshiriki katika kuangalia uandikishwaji wa kupitia teknolojia ya BVR, kura za maoni na uchaguzi mkuu wazingatie masuala ya usalama wao na kazi zao.
ii. Kusimama Imara na kuendelea kutetea haki bila kuogopeshwa na vitendo kama hivi vya hivi karibuni
iii. Kuungana kwa pamoja katika kusaidia wanachi kushiriki kikamilifu katika mambo makubwa ya kitaifa yatakayofanyika mwaka huu.
iv. Kuendelea kutumia fursa ya uwepo THRDC kujiweka sawa katika masuala ya usalama kabla ya kwenda kwenye uangalizi wa mchakato wa katiba na uchaguzi

**c) Kwa Wananchi /Umma wa watanzania**

i. Kutambua umuhimu wa waangalizi/AZAKI, na kutowaona kama ni maadui wa michakato ya kidemokrasia.
ii. Kudai uwajibishwaji wa askari polisi pale wanapovunja haki za binadamu na kutumia mabavu bila ya sababu.
iii. Kulaani vitendo vya askari vyote kama hivi vinavyokiuka haki za binadamu.

**MWISHO**

Tutambue kuwa mwaka huu ni mwaka wa mhimu sana kwa Taifa letu kwa Taifa litashuhudia matukio makubwa kama ya kura ya maoni pamoja na uchaguzi mkuu. Matukio haya yasiposimamia katika mizani ya haki na usawa kwa kuheshimu haki za raia, ni dhahiri kuwa hali ya usalama na amani itakuwa mashakani. Katika mazingira kama haya waathirika ni watetezi na waandishi wa habari, hivyo ni muhimu vyombo vya habari na AZAKI/Watetezi kuzingatia sana suala la usalama. Pia tunaomba vyombo vya dola vizingatie maadili ya kazi zao na kuepuka kuwa sehemu ya matatizo kwa kushidwa kuacha kuchukua upande mmoja hasa katika makundi ya kisiasa.

Imetolewa tarehe 16 Machi, 2015, Na:

**Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**



**Bw. Onesmo Olengurumwa**